

2235

95.147

WIDENER



HN JLJA N

MASOMO YA PILI

S.P.C.K.

5.95.147



Harvard College Library

BOUGHT FROM GIFTS

OF

FRIENDS OF THE LIBRARY

MASOMO YA PILI

MASOMO YA PILI

SWAHILI READINGS
COLLECTED FROM ARABIC STORIES
FOR USE OF THE UNIVERSITIES' MISSION TO CENTRAL AFRICA



SOCIETY FOR PROMOTING CHRISTIAN KNOWLEDGE,
LONDON: NORTHUMBERLAND AVENUE, W.C.

1904

2235.95.147

✓ HARVARD COLLEGE LIBRARY

THE GIFT OF
FRIENDS OF THE LIBRARY

OCT 28 1929

MASOMO YA PILI.

SEHEMU YA KWANZA.

KISA CHA MTU NA MWANAWE.

PALIKUWA na mtu na mwanawe, akamwambia babae, "Pesa zetu hizi tununue kuku tufuge, wakizaa tuwauze, tununue mbuzi, tufuge, wakizaa tuwauze tununue punda, akizaa unipe mimi nipande." Baba yake akamwambia, "Humpandi," "Nitampanda." "Humpandi." Wakagombana hatta akamtia kidole

cha macho, akamtoa jichomwanawe.
 Hawakupata punda, wala kuku.
 Hasara ikawafikilia, na pesa zao
 palepale. Wakajuta sana majuto
 makuu.

kuambia kununua kufuga
 kupanda kugombana kufikilia
 kujuta majuto

PAKA MTAWA.

Hapo zamani palikuwa na paka.
 Na bundi alikuwa Sultani, na
 paka akajifanya walii sana, hakamati
 nyama wala kitu kingine. Hatta
 siku moja panya akaenda kushtaki
 kwa paka, kwani ye ye amekuwa
 kadhi na walii. Paka akanena,
 "Sisikii sana, njoo karibu." Aka-

sogea panya, moyoni mwake anena,
 “ Hanikamati, mcha Muungu
 huyu.” Akasogea sikioni pake.
 Akamkamata. Akamwambia,
 “ Ginsi gani, mzee paka, utawa
 wako ? ” Akamwambia, “ Sijui.”
 Akamla.

Walii kukamata kadhi
 kusogea utawa kula

MWIVI NA KIATU.

PALIKUWA na mtu amechukua kondoo wake, akaenda hatta njiani akaona kiatucha mguu mmojakizuri sana. Akasema, “ Kiatu hichi kizuri wallakini kimoja tu, kakifai.” Akaenda zake. Hatta akafika mwendo wa nussu saa akaona kiatu

cha pili, namna moja na kile, aka-sema, “Nitafunga kondoo wangu hapa, nikatwae kiatu kile nilichokiona kwanza, na hichi nije hapa nichukue na kondoo wangu niende zangu.” Akamfunga kondoo wake pale, akarudi kwenda kutwaa kile kiatu kule. Akaona kiatu hapana, akarejea mbio kunako kondoowake, akaona kondoo hapana, wala kiatu hapana. Aliyekitia kiatu njiani ndiye mwivi akachukua kiatu na kondoo.

kuchukua wallakini kutwaa
kiatu kurejea mwivi

KAMBA NA JIWE.

PALIKUWA na mtu akaenda kusoma ilmu siku nyingi, asijue kabisa. Akafanya hasira, akaenda hatta akafika kati ya njia, akaona kisima, akaenda kutazama kana pana maji anywe, akaona jiwe la manga limekatwa na kamba, kwa sababu killa siku hupita katika lile jiwe. Aka-sema, Hii kamba imekata jiwe sababu killa siku kamba hupita juu yake, na mimi ntarudi nikasome, moyo wangu na uwe kama jiwe, na ilmu iwe kama kamba, ikate moyo wangu. Akarudi akasoma, akawa Shekh mkuu.

hasira	kisima	kunywa
ilmu	kurudi	kusoma

AYARI NA MTOTO:

PALIKUWA mtu mmoja ayari, akidanganya watu. Bassi akamwambia mtoto mmoja, "Njoo, fanya kazi kwangu, mwezi 'takupa reale miteen, lakini mwezi ukiisha 'takutuma ulete vitu viwili, ukileta, bassi reale miteeni 'takupa. Hakuna kuleta, hakuna kupa." Bassi yule akasema, "Ee Walla !" akakubali.

Bassi akakaa kwakehatta kutimia mwezi, akamwambia. "Umekwi-sha mwezi, nitume nikuletee vitu viwili, nipate fedha yangu." Akamwambia, "Kalete Ha-a ! Hi-i ! 'takupa reale miteen. Nenda zako."

Bassi yule akafikiri, "Ha-a ! Hi-

i! nini?" Åkaenda akatafuta tandu. Akamkamata tandu kubwa, akatia ndani ya chupa nyeusi. Akatafuta tena nge kubwa, akaitia ndani ya chupa. Akafunga vema. Bassi akampelekea. Akamwambia, "Hii Ha-a! Hi-i!" Yule akatazama chupa. Akasema, "Nini ndani yake?" Akamwambia, "Tia kidole." Bassi yule akatia kidole. Akamuma kidoleni yule tandu. Alipomuma akasema, "Ha-a-a-a! Ha-a-a-a!" Akasema, "Ee, umeiona Ha-a? Hi-i imo ndani ya chupa!" Bassi akatoa reale miteen.

kudanganya	Ayari	kutuma
kukubali	kutimia	fedha
reale	kufikiri	kupelekea
miteen		

KUZIKWA KWA FISI.

FISI alikuwa na mkewe, akazaa nae watoto wawili. Akakaa baada yake, akafa mkewe, akabaki yee na watoto wake.

Bassi killa siku assubui huwaambia watoto wake, “Nakwenda kuzuru katika kaburi ya mama yenu.” Bassi huenenda kuzuru, afikapo katika kaburi humfukua mkewe akimla. Kill a siku kazi yake hiyohiyo.

Wale watoto wakitaajabu, “Gissi gani huyu mzee wetu hunena, nakwenda kuzuru ? Bassi kuzuru huko gissi gani ?” Hatta siku moja alipoaga, kama “Nakwenda kuzuru,” wakamfuata nyuma, waka-

enda, wakamwona anamfukua mke wake, mama yao, akimla. Waka-rudi wale vijana, wakanena ; “ Kuzuru kwa baba anapomzuru mama vizuri ! ”

Bassi akakaa. Alipokuwa mzee akawausia waanawe, akawaambia, “ Enyi waanangu, ’tawausia : nikifa nizikeni sana, mnifanyie kulla jambo jema.” Wale watoto wakamjibu baba yao, “ Kuzikwa kwa fisi si kiwiliwili tu ? ”

kubaki	kuzuru	kaburi
kufukua	kutaajabu	kuwusia
kuzika	kiwiliwili	

KUTOKA KABURINI.

PALIKUWA na mtu mwanamume akaenda kuoa kijana mzuri sana wakapendana sana. Hatta walipokuwamo nyumbani mwao mwanamume akamwambia mwanamke, "Mimi nakupenda sana siku nitakayokufanitakutokea." Mwanamke akamwambia vilevile. Baada ya siku nyingi yule mwanamume akaugua, akafa. Wakaja watu wengi, wakalia sana. Na yule mwanamke akalia akitumaini yale maneno waliyoahidiana. Yule aliyeckufa akaenda kuzikwa, lakini mwanamke hakukubali kurudi pamoja na watu. Watu waliporudi akabaki yeche peke yake kaburini,

anakwimba tu peke yake. Akaona udongo wa kaburi unapasuka, aka-mtokea. Yule kijana alipomwona akafurahiwa sana, wakaenda zao hatta nyumbani. Bassi mama yake yule mwanamke aliweka msiba, hatta jioni akamsikia yule kijana mwanamke anacheka kwa furaha kuu. Mamake akaja, akamkemea, akamwambia, “Unacheka nini? mume wako amekufa.” Akamjibu, “Hakufa, yuko ndani.” Akaingia ndani mama yake akamwona kweli. Baada ya siku kidogo akaugua yule kijana mwanamke, akafa. Watu pia wakalia, lakini mume hakulia, akanyamaza tu. Hatta akaenda akamzika, waliporudi watu yule kijana mwanamume hakurudi. Akatoa ushuhuda akiimba, akaona

kaburi linapasuka. Akatoka yule mwanamke, wakaenda zao hatta nyumbani kwao. Hatta jioni akaja yule yule mama yake mtoto mwanamke, akawakuta wote wawili, wanakaa mlangoni. Akaenda zake kwa furaha. Watu walipowaona wakafurahi. Ndio mwisho.

mwanamume	kupendana
kutokea	kuugua
kutumaini	kuahidiana
kuimba	kupasuka
kukemea	kunyamaza

MJAKAZI MTAWA:

PALIKUWA na mtu, akanunua mjakazi kwa ashrat alaf dinar, aka-kaa akimtezama mjakazi wake, aka-

lia sana. Yule mjakazi akamwuliza, “ Unalilia nini bwana wangu ? ” Akamwambia, “ Macho yako mawili, killa nikiyatazama hunishughulisha, hatta katika ibada ya Mola wangu siwezi kuabudu kwa uzuri wa macho yako.”

Akatoka yule bwana ; yule mjakazi akayatoa macho yake yote mawili kwa kidole, akayatupa. Alipokuja bwana wake akamwona hali ile na macho hana akamwambia, “ Kwa nini ukafanya hivi ? ” Akamwambia, “ Mimi sipendi ne-no ambalo litakushughulisha hatta katika ibada ya Mola wako.”

Akamwambia, “ Nimekununua kwa asharat alaf dinar ; sasa ukiwa hali hii sitapata fedha yangu, imetoka thamani yako.” Akalia sana yule

bwana wake akafanya huzini.
 Hatta ukawa usiku akalala,
 akamjia hatif akamwambia, "Sasa
 huyu ameivunja thamani yake
 kwako, bassi sisi tutamnunua,
 utaiona thamani yako chini ya mto
 wako." Hatta alipoamka assubui,
 akafunua mto akaona fedha zake,
 akamtazama mjakazi amekufa.

**mjakazi kushughulisha ibada
 thamani kuamka assubuhi**

HEKAYA YA MTUME.

PALIKUWA na mtume akiabudu
 katika jabali kubwa, na chini yake
 pana maji yanapita, na wakati wa

mchana, hukaa juu ya jabari, wasipate kumuona watu. Hatta siku moja amekaa anatazama mto wa maji, akamwona mtu anakuja, aka-shuka juu ya farasi wake, akaweka mfuko uliokuwa begani mwake, akastarehe akanwa maji, kisha akaenda zake, akauacha mfuko wafedha. Marra akaja mtu mgine, akaona mfuko akautwaa, akanwa maji akaenda zake na furaha. Akaja mtu mgine mchanja kuni, nae amechukua mzigo wa kuni mzito juu ya mgongo wake, akakaa mtoni, akanwa maji. Marra yule wa kwanza mwenye fedha akaja mbio, akamwambia mchanja kuni, “Uko wapi mfuko uliokuwapo hapá?” Akanena, “Sijui, wala sikuona.” Yule akatwaa upanga

akampiga mchanja kuni, akamua. Akamtazama nguoni mwake, asione kitu. Akamwacha, akashika njia akaenda zake. Akanena yule mtume, “Ee Muungu wangu, aliyechukua fedha mtu mgine, na aliyeuawa mgine, amedhulumiwa yule.” Mwenyiezi Muungu akamshushia walii akamwambia, “Wewe tazama ibada yako, na ukitaka mambو haya, si kazi yako.” Akamwambia, “Baba yake yule wa kwanza alimnyang’anya dinar alf katika mali za babae yule kijana, hamleta yule kijana kuja twaa mali ya babae. Na yule mchanja kuni alimua babae yule wa kwanza, hamleta kijana kuja kutoa kisasi cha babae.” Akanena yule mtume, “Hapana anaeabudiwa kwa haki, illa wewe, uliyepuka-

na na maovu, nawe ndiwe unaejua
ghaib."

kuabudu	farasi	mgongo
mchanja	kudhulumiwa	
kushushia	kunyang'anya	
kisasi	kuepukana	ghaib

ZAMANI ZA NABII DAUD.

PALIKUWA na kizee mwanamke,
killa siku kazi yake kufanya mikate
akapeleka mosikitini. Hatta siku
moja akasaga unga wake, akaweka ;
ikaja baridi, ikachukua unga wake
wote. Akatoka kwenda kwa nabii
Daud kuishtaki baridi, imemtwalia
unga wake. Hatta njiani akam-

wona Nabii Sulemani. Akamwuliza, "Unakwenda wapi, wee kizee." Akamwambia, "Nakwenda ku-shtaki kwa baba wako, baridi imenichukulia unga wangu." Akamwambia, "Nenda." Akaenda hatta kwa Nabii Daud akashtaki kwa sababu ya baridi Akampa asharat alaf dinari. Akarudi, akamwona Nabii Sulemani, akamwuliza, "Habari zako?" Akamwambia "Baba yako amenipa asharat elf dinari." Akamwambia, "Hii siyo haki yako, amekupa sadaka, enenda marra ya pili, akakutolee haki yako." Akaenda marra ya pili akampa fedha vilevile. Akarudi akamwona Nabii Sulemani, akamwambia, "Hii fedha siyo haki yako, enenda tena." Akaenda

marra ya tatu akampa fedha vilevile. Akamwona nabii Sulemani, akamwambia “ Na sasa amenipa fedha vilevile.” Akamwambia, “ Hii siyo haki yako, enenda ukamwambie nitozee haki yangu kwa baridi, kumwaya unga wangu.” Akaenda. Akamwambia, “ Nani huyu anaokuleta huku marrakwa marra.” Akamwambia, “ Mwanao Nabii Suleman.” Akamwambia, “ Nataka haki ya Muungu naishktaki baridi utuhukumu kwa haki.” Nabii Daud akaita baridi, ikaja. Akaiuliza kama. “ Kwani ukamwaya unga wa huyu maskini.” Akamwambia, “ Si mimi, nimetumwa na Israfil.” Akamwita Israfil, akamwambia “ Kwani ukaamuru baridi kumwaya unga wa huyu maskini ? ” Akam-

wambia, “ Mimi nimetumwa na Mungu wako, Mungu haharibu neno illa kutengeza neno. Pali-kuwa na marikebu, imepata watu thelathini elf, ikatoboka nao wako katika bahari. Bassi nikaamuru baridi kuchukua unga, kwenda nao hatta panapo marikebu pamoja, ukaenda ukaziba tundu ya marikebu Ikiwasili hiyo marikebu ; theluthi ya mali, mpeni huyu maskini mwenye unga.” Ilipowasili marikebu akapewa maskini haki yake, theluthi ya mali.

moskiti	kusaga	baridi
kushtaki	kuwaya	kuhukumu
kuamuru	thelathini	kuharibu
kutoboka	kuwasili	marikebu
maskini	theluthi	

KISA CHA WAZIRI NA SULTANI WAKE.

Hapo kale palikuwa na Sultani na waziri wake. Wakapendana sana, hatta yule waziri akafanya paa wa dhahabu akampelekea Sultani wake. Yule Sultani akatwaa yule paa akamweka miguuni mwake, wakakaa yeye na waziri wake. Marra akatokea Shekh alim, yule Sultani alipomwona yule Shekh akafadhaika, akamsahau yule paa akaondoka. Akaanguka yule paa akavunjika. Yule waziri akafanya hasira sana, akanena, "Mimi waziri, tena tajiri, amekuja huyu masikini, nami nimefanya hedaya, huyu paa, Sultani amefadhaika, ameanguka

paa wangu amevunjika. Si hii ilimu kitu bora sana? Nitamngojea akiondoka nimfuate hasome ilmu.”

Alipotoka yule Shekh akamfuata. Akamwambia, “Hutaweza kusoma.” Akamwambia, “Enenda mahali fullani pana tope, twaa upake ndevuni mwako.” Akamwambia, “Vema.” Akatoka akaenda, na yule Shekh akamwambia mtu wake, “Enenda mfuate, ukimwona ataka kupaka, mkataze, mlete huku.” Akamfuata, akamwona ataka kupaka, akamwambia. “Shekh anena, Bassi.” Wakaja hatta kwa Shekh akamsomesha ilmu, akawa Shekh bora, akaitwa Imam il ghazal, kwa sababu ya paa wake wa dhahabu.

Akaja kwa Sultani wake, na mbele ya nyumba ya Sultani pana jabali kuu, akitaka kutoka shurti azunguke. Akamwambia, "Wewe kana Shekh kweli nataka uliondoe hili jabali hapa mlangoni pangu, kama hukuweza nitakuua." Akamwambia, "Wallakini shurti ushike mwenyewe mtaimbo upande juu ya jabali ukalipige kidogo kidogo." Akatwaa mtaimbo yule Sultani, akapanda juu ya jabali akalipiga, na yule Shekh akalisomea jabali hatta likachezacheza lile jabali. Akamwambia, "Kaa vema katikati." Akakaa yule Sultani na yule Shekh akalisomea jabali, likaruka na Sultani pia, asitambulikane alikokwenda. Watu wakamuza habari, akawaambia, "Sul-

tani yule alitaka kuniua, nami ni-memua yeye.”

waziri	dhahabu	kufadhaika
kuanguka	kuvunjika	tajiri
hedaya	kungojea	kuondoka
ndevu	jabali	kusomesha
mtaimbo	kutambulikana	
kuzunguka		kucheza

KISA CHA MTU NA NDUGUYE.

PALIKUWA na Sultani na nduguye, na yule nduguye alikuwa masikini ; wakitafuta chakula, hawakipati, yeye na mkewe. Hatta siku moja aka-fanya shauri na mkewe, kutoka mji sababu ya umasikini. Wakatoka mji, yeye na mkewe na waanawe

pia, wakaenda hatta mji wa pili. Wakafika mahali chini ya mti, wakakaa, wakapumzika. Na juu ya mti pana jini. Akauliza, "Enyi waana Adamu, mwatendani hapo?" Wakamjibu, "Sisi twakutafuta wewe, mwaka wa tano huu, na leo imetimia ajali yako. Sisi tuna njaa, tutakupika." Akawatuma watoto wake, mmoja akaenda akaleta kamba, na mmoja akaenda akaleta moto. Akamwambia mkewe, "Teleka sufuria." Akateleka sufuria, wakamwambia, "Leo utaona wee shetani." Akamwambia, "Msiniue bali twaeni hii sufuria; kwa killa kitu mkitakacho itawapa hii sufuria." Akawapa sufuria.

Wakaenda zao hatta mjini mwao, killa wakitaka kitu hupata katika ile

sufuria. Wakaonekana nyumba yao haifuki moshi. Hatta yule mkewe siku moja akaenda kule kwa nduguye mumewe. Yule akamuza “Ninyi kwanza mlikuwa mkiomba, sasa kwani hamwombi?” Akamweleza habari toka mwanzo hatta mwisho. Na yule akamwambia mumewe, “Bwana nasi twende tukatafute.” Wakatoka wakaenda hatta wakafika palepale. Akawona akawauza, “Mwatakani?” Wakamwambia, “Twakutafuta wewe.” Yule Sultani akawaambia waanawe. Wakamwambia, “Tumechoka, hatuwezi kwenda kutafuta kuni na kamba.” Akamwambia mkewe “Teleka sufuria mekonî.” Akamwambia “Nimechoka.” Yule shetani

akawaambia, “ Hamwezi nyie, mwataka kufa bure, hatta shauri yenu si moja, rudini inchini mwenu, na killa samli mkifanya mpelekeeni yeye.” Wakarudi mbio hatta mjini mwao, hasara ikawajilia, killa wakifanya samli humpelekea nduguye, kwa sababu ya tamaa yao.

mkewe	shauri	umasikini
kupumzika	jini	kuuliza
ajali	kuteleka	sufuria
shetani	kufuka	kuomba
kueleza	mwisho	mekoni
kutafuta	samli	kujilia
hasara	tamaa	

KISA CHA MWANA WA SULTANI.

PALIKUWA na mwana wa Sultani akarithi mali mengi, nae alikuwa karimu sana, yakampotea mali yake pia, kwa sababu ya ukarimu wake, akaona fedheha, akafanya shauri ya kutoka mji. Akatokaakaenda hatta akafika mji wa pili, akaona kisima akachungulia ndani ya kisima, akaona simba na nyoka na mwanadamu. Wakamwambia, “Tufae, nasi tuje tukufae.” Akawatoa simba na nyoka, wakamwambia, “Ewe bin adamu, twakupa wusia wetu, Mwanaadamu hatendwi mema, ukimtenda mema yeye hukulipa maovu.” Akamtoa na

yule bin adamu. Yule simba aka-mwambia, "Ningoje, ewe mwana adamu." Akaenda yule simba hatta karibu na mji, akamwona binti wa Sultani akamkamata, watumwa wakakimbia, akamletea yule kijana na tunza zake, akamwambia, "Twaa hivi yote, mimi nipe huyu kijana nimle." Akamwambia, "Kama utanipa, nipe na huyu kijana pia." Akampa. Akamjengea kibanda aka'mweka. Na yule nyoka akamtolea meno yake mawili, akamwambia, "Ukipatikana na shaka, twae jiwe uyagonge, Insha'allah'ta-kutokea marra." Mle mjini watu wanamtafuta mwana wa Sultani, hatta siku moja yule kijana amekwenda kupiga ndege, akaja yule mtu aliyetolewa kisimani hatta

panapo nyumba ya yule kijana akamwona mtoto wa Sultani, akapiga mbio akaenda kuwaita watu mjini, wakaja, wakamwona mwana wa Sultani na yule kijana. Wakamtwaawakamfunga, wakaenda nae hatta kwa Sultani, akatwaliwa akafungwa pasipo mtu wasimpe chakula. Hatta watumwa wengine wakimwibia vipande vya mkate wakimpa akila. Hatta siku moja akanena, “Tajaribu nikatwae jiwe nigonge.” Akagonga yale meno na jiwe, marra akatokea nyoka akamwambia, “Mimi leo Sultani akienda koga, nitamura hatapona ela kwa meno yangu.” Akaenda kukaa juu ya birika. Alipokuja Sultani, akampiga mdomo, akaanguka Sultani chini.

Wakaja watu wakamchukua, wakaisha watu kufanya dawa asipone kabisa. Akanena, "Mtu atakaeweza kunifanyia dawa nikapona nita-mwoza binti yangu nitampa upande wa mji." Akaja kizee akamwambia, "Mimi nimetazama nimeona hapana mtu atakaeweza kufanya dawa ukapona, ela yule mtu aliyefungwa, kamtoeni aje." Wakaenda wakamleta. Akamwambia, "Mimi sijui dawa." Akazunguka akayasaga yale meno, akampa yule Sultani, akapaka. Siku ile marra alipata usingizi. Akamuza habari zake. Akampa habari toka mwanzo hatta mwisho. Akatwaliwa mwana adamu yule akashonewa fumba, akatoswa baharini. Yule kijana akapata daraja

bora, akaozwa binti wa Sultani,
akakaa raha mustarehe.

kurithi	karimu	fedheha
kuchungulia	kukamata	tunza
kujengea	kupatikana	
kugonga	birika	
usingizi	koga	
kushonewa	kutoswa	

KULETA MVUA.

PALIKUWA na mtu. Akapata vijana wawili, mmoja mkubwa, na mmoja mdogo. Baba yao na mama yao wakafa. Hatta ile inchi ikakauka maji pia ; vyakula tele, maji hapana. Na palikuwa watoto walikuwa wakicheza wa-

kichukua unga na vijungu, yule kijana mwenye hana mama akawaambia wenziwe, “ Nitawaambia neno, nanyi msimwambie mtu.” Wakamwambia, “ Hatusemi.” Akasema, “ Leteni mitungi yenu hapa.” Wakaileta. Na yule mtoto akasimama katikati yao, akatazama mbinguni. Akaona wingu dogo likakusanyika. Ikaanguka mvua pale pale walipo. Wakapika vyakula vyao. Wakala, nussu wakapeleka mjini. Baba zao wakawauliza, “ Maji mmeputa wapi ? ” Wala hawakusema wakanymaza tu. Siku ya pili wakaenda wakakutana pale pale. Yule kijana akawauliza, “ Nani aliyekwenda kusema ? ” Wakasema, “ Hapana mtu.” Akawaambia, “ Leteni

mitungi yenu." Na kijana mmoja mjanja sana, akaleta mitungi miwili. Yule mtoto akasimama tena katikati - yao akitazama mbinguni, akaona wingu nene linakuja, ikanya mvua nydingi sana pale pale, wala hai-kufika mjini. Na yule mtoto mjanja ilipokuwa ikinya mvua akakinga mtungi mmoja, akaenda kuficha maguguni. Walipokwisha kupika wakaenda zao. Hatta ulipokuwa usiku watu wote wamelala, akamwita mama yake akamwambia, "Nitakwambia neno, usimwambie mtu." Akajibu, "Nambie mwanganu." Wakatoka wakaenda hatta alipoficha mtungi wa maji akauchukua, akaja nyumbani mwake. Akampeleka yule, na yule akampeleka mwenziwe hatta wakafika kwa

Sultani. Sultani akawaita waziri wake, akawauliza, "Maji yametoka wapi?" Akamjibu "Kwa yule mtoto wa masikini." Mji mzima pia wakachimba visima. Hatta vili-pokwisha Sultani akamwita yule mtoto mwenye kuleta maji, akaampa vyombo vyat dhahabu waka-mpeleka barazani. Watu pia wa-kakusanyika pale pale. Sultani akamwambia, "Ulete mvua." Yule mtoto akamjibu, "Jogeni mbali." Wakakataa pia wote. Hatta yule mtoto akata-zama mbinguni akaona mawingu tele mengi, ikanya mvua nyingi sana. Ukanguruma umeme na radi, akachukuliwa yule mtoto mbinguni. Na wale waliopo wakamtazama mtoto, hapana,

wakaachiwa maji mengi sana.
Ndio mwisho.

kukauka	mtungi	mbingu
kukusanyika	kukutana	mjanja
kukinga		maguguni
kuchimba		barazani
kunguruma		umeme
kuachiwa		radi

NABII MUSA NA MTU MASIKINI.

MTU mmoja alikuwa masikini,
hatta pesa moja hapati. Akienda
akiomba, hupata chakula tu bassi,
hatta miaka arobaini hakupata robo
moja, licha reale. Akaenda ąkakaa
njiani kungoja nabii Musa akipita.

Nabii Musa akamwona. Aka-mwambia, "Ee ! Mtume wangu, tafadhali unapokwenda kwa Bwana wetu Mungu, nisalimie Bwana wangu. Mwambie, kwani hutaki kumruzuku mtumwa wako, amekosa nini ?" Nabii Musa akamwambia, "Marahaba." Akaenda Musa akapanda jabali, akajizungumza na Bwana wake, hatta alipokwisha kuzungumza, akataka kushuka. Mwenyezi Mungu akamwambia Musa, "Kwa nini wewe, kupewa amana, usimpe mwenyewe ?" akanena nabii Musa, akamwambia Mungu, "Wewe ndiye usiosahau ; mimi nilipewa salamu kukuletea na mtumwa wako. Akwambia, kwa nini hutaki kumruzuku ?" Mungu akamwambia nabii Musa, ya

kwamba “ Kanisalimie, umwambie, simruzuku kabisa.” Akarudi nabii Musa katika jabali, akamwona yule mtu aliomtuma. Yule mtu akamwambia nabii Musa, akamwuza, “ Je ! amekujibuje ? ” Nabii Musa akamwambia, “ Salamu, Bwana wako. Baada ya salamu, anena ya kwamba hakupi, hatta pesa moja.” Yule akalia, akarudi, akaenda zake. Siku ya pili akaenda akamkalia nabii Musa katika njia ileile hatta akamwona anakuja nabii Musa, akamwambia “ Ewe ! Mtume wa Muungu, tafadhali ukienda nisalimie Bwana wangu ; umwambie tafadhali mruzuku mtumwa wako.” Akalia yule mtu kwa nabii Musa. Akamwambia ya kwamba, “ Tamwambia Bwana wetu.” Musa

akapanda katika jabali akaenda kusema na Bwana wake hatta alipokwisha kujizungumza na Bwana wake, alipotaka kushuka akasahau maagizo aliyoamriwa na yule mtu. Muungu akamwambia nabii, “Kwa nini wewe kupewa amana usimpe mwenyewe?” Akanena nabii Musa ya kwamba “Wewe Mungu ndiye usiosahau mambo yote. Mtumwa wako amenipa salamu.” Akamwambia, “Hali yake dhaifu, ataka umruzuku.” Mungu akamwambia nabii Musa ya kwamba, “Mimi sipendi kumpa mali, wallakini sasa ‘tamruzuku reale moja tu yule.” Musa yuko kulekule juu ya jabali.

Yule mtu akapata reale moja.

Alipopata reale, akanena yule mtu, “ Reale hii nitakwenda kununua upanga.” Akaenda sokoni akaenda kuona upanga. Akaona upanga unatembezwa kwa reale. Akam-wuliza “Kassi gani upanga huu ?” Akamwambia, “Reale.”

Akampa reale, akatwaa upanga, akaufuta. Alipoufuta akanena ya kwamba, “Upanga huu mtu kupi-gana na mtu hivi !” Akampiga mtu akafa, nae akauawa. Mwe-nyezi Mungu akamwambia nabii Musa, “Shuka umwangalie mtu wako.” Akaenda, akamwona amekufa. Mungu akamwambia nabii Musa ya kwamba “Mimi sikupenda kumfanyia hivi kumpa mali; mimi nalipenda awe masikini, lakini leo umemtakia mali, na mali

jana madhara yake. Sasa amekufa."

tafadhalii kuruzuku marahaba
jabali kuzungumza
mwenyewe wallakini
kutembeza kufuta
madhara

HADITHI YA WATOTO NA ZIMWI.

PALIKUWA na watoto, wakaenda zao mtoni kutafuta kauri. Mmoja akapata kauri moja, akaiweka jiweni. Wakatafuta, wakapata, wakaenda zao. Yule mtoto akasahau kauri yake, akawaambia, "Nimesahau kauri yangu nzuri sana, twendeni mnipeleke nikatwae kauri yangu."

Wakamwambia, “Nenda ukatwae tutakungojea,” akaenda akiümba.

Cheche cheche chambalamanda,

Ngala jangu naliwele,

Nati mbuje ngatole.

Kwasimama andamilile

Wati lutumbo kuchukuchu.

Akamkuta zimwi amekaa kitako katika jiwe, akamwambia, “Taka nini?” akaimba, akamwambia, “Njoo sisikii, njoo karibu.”

Akajongelea karibu, akamtwa, akamtia ndani ya pipa, akamchukua, akaenda nae akakuta watu wamekaa barazani, akawaambia, “Nina ngoma yangu, nataka kuku na wali nile.” Wakamwambia, “Imba,” akaimba yule mtoto. Zimwi aka-pewa chakula, akala, wala mtoto yule hampi, anakula ye ye mwen-

yewe. Zimwi akaenda mji wa yule mtoto, watu wakasema, "Tumesikia kama Zimwi una ngoma nzuri sana, twimbie."

Akasema "Nataka pombe." Mtoto akaimba, watu wote wakasema, "Huyu mtoto wetu." Wakampa Zimwi pombe akalewa akalala. Wakaenda watu wakaitwaa ngoma yake wakamwona mtoto wakamchukua, wakamficha chumbani ; mle ndani ya ngoma wakatia nyoka na nyuki na maji ya moto, wakafunga vilevile. Wakaenda wakamwamsha wakasema, "Zimwi amka ! watu wamekuja wanataka ngoma yako." Akaitwaa ngoma yake, akaipiga akasikia kimya, hakusikiasautiya mtotoyule. Zimwi akaenda zake hatta njiani akafungua

ngoma akaona nyoka, ikamuma akafa. Pale alipokufa pakaota maboga na matango. Wakaja watoto wakasema, "Maboga haya mazuri. Twende tukatwae upanga wa baba tuje tuyapige." Boga moja likaona hasira likawakimbiza wale watoto, wakakimbia, wakaona mto, wakamwona kizee wakasema, "Ewe baba tuvushe, tupeleke hatta ng'ambu ya pili, tunakimbia boga." Yule kizee akawavusha, wakakimbia wakaona mji wa pili wakafika wakakuta watu tele barazani wakawaambia, "Tuficheni boga lile, Zimwi amegeuka boga, bassi litwaeni mlichome moto." Likaja lile boga likawaambia, "Mmeona watu wangu wanaokimbia" Wale watu wakasema,

“Watu wako gani, hatuwajui.” Likasema “Mmewafungia ndani.” Wakatwaa boga, wakatia moto tele, boga likaunguzwa likawa majivu, wakayatupa. Wakafunguliwa watoto, wakaenda zao kwa mama zao.

kungojea kujongelea barazani
kulewa kuamsha kuvusha
kuficha ng’ambu
kuunguzwa majivu

SEHEMU YA PILI.

HADITHI YA MWIZI NA TAJIRI.

INCHI ya Misri, siku moja usiku saa saba aka-toka mwizi, akachukua sanduku yake akaenda hatta nyumba ya tajiri, akabisha mlango aka-fungua akaingia, akamuza, "Nani wewe?" Akamwambia, "Mimi nalikuwa mwizi mkuu, sasa nataka kutubu kwa Mola wangu, twaa hii sanduku yangu, nipe asharat alaf dinar, halipe mali za watu nilizokwiba." Akafungua sanduku akaona johari, na yakuti, na feruzi, na almasi, akafurahi yule tajiri, akatwaa asharat alaf dinar, akampa akaenda zake. Yule tajiri usiku kucha asilale kwa furaha ya mali. Hatta assubuhi akafungua, akatazama, akaona vigai vitupu. Akalia sana, na mwizi hamjui akavitupa vigai. Mali yamepotea, hayapati tena kabisa.

Misri sanduku tajiri kutubu
johari yakuti feruzi vigai

SHEKI NA MLEVI.

ALIKWENDA mwana wa chuoni mkubwa kute-mbea katika mji. Alipowasili mjini, hakuingia ndani aliketi nje mashamba. Wakaondoka watu wa mji kwenda kumtwaa wamlete mjini. Akakataa akanena, "Nna maswali yangu ; mkinijibu ntaingia ndani ya mji." Wale watu wakamwuliza, "Maswali gani ?" Akawaambia, "Hivi," akinyosha kidole kimoja. Wale watu hawakujua, wakarudi mjini. Wakaondoka watu wengine tena kwenda kumtwaa. Wakamwambia, "Twende zetu mjini," akakataa, "Siendi, ela mnijibu swalilangu." Wakamwuliza, "Swali gani ?" Akanyosha kidole. Hawakujua watu. Wakarudi. Bassi wakaenda watu wengine tena wengi. Na killa waendao aka-wauliza vilevile. Wakarudi wasijue, hatta watu wote wakaisha. Wakashindwa watu hawakuweza kumtia ndani ya mji.

Akaondoka mtu mmoja mlevi, akawaambia, "Mimi nitamleta, ninyi watu wakubwa wa mji, hamwezi kumleta, nami nitamleta." Watu wakamjibu, wakamwambia, "Watuhakubwa wenye mali hawawezi kumleta utamleta wewe ?" Akasema, "Tamleta." Akaenenda akafika kwyule mwana chuoni, akamwambia, "Siendi ela

unifungulie maswali yangu." Akamwambia, "Nambie maswali yako." Akamwambia, "Hivi." Akanyosha kidole kimoja. Na yule mlevi akafanya hivi, akanyosha vidole viwili. Yule mwana chuoni akafanya hivi, akapunga mkono kwa juu. Na yule mlevi akafanya hivi kwa chini. Yule mwana chuoni akafanya hivi, akashusha kidole cha katikati tangu juu hatta chini. Na yule akatoa kidole cha kati kwenda juu. Mwana chuoni akampa mkono yule mlevi, akamshika mkono wakaenda zao mjini. Akawaambia watu, "Huyu mwana chuoni nime-mleta." Watu wakaona ajabu kuu, watu havakuweza, nae amemleta. Watu wa mjini wakamfanyia karamu mwana chuoni wakampa nyumba, wakamweka. Hatta alipopumzika siku mbili wakatoka watu wenye akili kwenda kwa mwana chuoni kumwuliza, "Alifunguaje maswali yako akulete mjini."

Mwana chuoni akawaambia, "Alikuja kuni-leta mjini hakataa, hamwambia, 'Sharti unifungulie maswali yangu, ndipo nitaingia.' Akaniambia, 'Nini maswali yako?' nambie. Hamwambia 'Muungu ni mmoja' ndiyo maana ya kidole kimoja. Naeakanijibu, 'Na mtume wake,' ndiyo maana ya viwili. Hamwambia, 'Muungu ametandika mbingu.' Akajibu, 'Na Muungu akatandika inchi.' Hamwambia,

‘Muungu hushusha mvua.’ Akanijibu ‘Muungu hutoa mimea.’ Bassi hampa mkono tukaingia mjini.” Watu wakawendea tena yule mlevi wakauliza, “Na yule mwana chuoni umemfunguliaje maswali yake.” Akasema “Nikamwambia, ‘twende mjini,’ akakataa, akaniambia, ‘Sharti unifungulie maswali yangu ndipo naenda mjini.’ Hamwambia, ‘Niambie maswali yako.’ Akanambia, ‘Shujaa ni mimi peke yangu.’ Nami hamjibu, ‘nami wa pili.’ Akaniambia, ‘Takukata kitwa,’ nami hambia ‘takukata mguu.’ Akaniambia, ‘Takutia chanda cha utosi.’ Nami hamwambia, ‘Takutia cha chini.’ Bassi akanipa mkono tukaingia mjini.”

kutembea	Maswali	kunyosha
mlevi	kupunga	kupumzika
kutandika	utosi	

SUNGURA NA MGOMBA.

PALIKUWA Sultani, na katika mji wake maji hapana. Bassi akawakusanya nyama zote za killa namna, kuchimba kisima. Lakini Sungura akasema, “Mimi sitaki kuchimba.” Waka-

mwambia Sultani, "Sungura hataki kuchimba." Sultani alisema, "Bassi mwacheni, chimbeni wenyewe." Wakaenda. Walipokwisha wakaenda kuteka maji. Bassi mwanamke wa Sungura akasema, "Tutakunywa nini, tapata maji wapi?" Sungura akasema, "Haidhuru, tutapata maji." Bassi wote wakasema, "Ngojeni hapa, tutamkamata Sungura."

Lakini Fisi akasema, "Nitakaa peke yangu nitamkamata marra moja." Akakaa, hatta saa tatu ya usiku akamwona Sungura anakuja na vibuyu vyake, kimoja kikavu na kimoja chenyi asali. Akapiga hodi akasema, "Mimi sitaki maji nataka kupita tu." Fisi akasema, "Kama hutaki maji, pita bassi." Sungura akasema, "Maji yangu matamu, yako mabaya, sitaki maji yako." Fisi akamwambia, "Nipe kidogo maji yako niyajaribu." Akatia kidogo kinwani mwake. Fisi akalia akisema, "Ongeza, ongeza, yako matamu, kweli matamu sana." Sungura akasema, "Huna buddi kufungwa sana na mti kwanza kwa sababu utaanguka." Fisi akasema, "Nifunge bassi, nifunge na ongeza maji yako, lakini usinifunge sana." Akamfunga hodari sana. Alipokwisha kumfunga, Fisi akasema, "Nipe maji yako." Lakini Sungura alicheka akampiga sana, akateka maji, akamwacha kule-kule mtini.

MASOMO YA PILI

Bassi assubuhi na mapema wote walikuja kumtazama yule Fisi, walipomwona wakasema, "Unafanya nini Fisi wee?" Akasema "Wengi wamenifunga." Simba akamwuliza, "Wangapi?" akasema, "Wengi, wengi." Simba akasema, "Unasema uwongo wee, mmoja tu Sungura kakufunga." Bassi wakamfungua wakarudi katika mji. Simba akasema, "Nitakaa usiku huu nitamkamata." Bassi akakaa, akakaa hatta saa tano ya usiku.

Sungura alikuja akapiga "Hodi! hodi kisima!" Lakini Simba akanyamaa kimya vile-vile. Sungura alisema, "Bassi nitateka maji ya kuoga tu, sitaki maji ya kunywa, maji yangu matamu." Simba alikaa vilevile.

Sungura akatwaa kata kuteka maji, Simba akaruka akamkamata, Sungura akalia akisema, "Mimi sitaki maji, sitaki kabisa maji yako, maji yangu matamu." Simba akasema, "Nipe kidogo," Akatia kidogo kanwani mwake, akanywa akisema, "Kweli matamu, nipe tena, ongeza." Sungura akasema, "Haifai, huna buddi kufungwa sana na mti, kwa sababu utaanguka." "Nifunge bassi na ongeza." Akamfunga hodari. Alipokwisha kumfunga akasema, "Nipe bassi." Akajibu, "Mpumbavu wewe?" Akateka maji, akaoga ndani ya kisima akaenda zake.

Tena assubuhi na mapema wote walikuja kutazama kama Simba amemkamata. Lakini Fisi akamwona akamcheka sana akasema, "Ati wengi wamekufunga wewe, Simba ?" Simba akasema, "Bassi usiseme amenishinda." Wakamfungua.

Kobe akasema, "Nitamkamata, nitakaa usiku huu." Bassi akaingia ndani ya maji akakaa chini. Sungura alikuja akapiga "Hodi ! hodi kisima ! nini hii ? hapana mtu hapa leo ?" Kobe akanyamaa kimya. Sungura akasema, "Bassi nitateka maji." Akatia mkono wa kuume, kobe akamkamata, Sungura akalia sana, "Nani wee ? mimi sitaki maji, maji yangu matamu, niache, ujaribu." Lakini kobe akanyamaa kimya akamshika hodari. Sungura akatia mguu, akatia miwili, akamkamata.

Sungura akalia akajaribu kuondoka, lakini kobe akamshika hodari sana. Tena assubuhi walikuja wote, wakamwona Sungura, wakasema, "Sungura ameonekana leo, tutamfunga na tutampeleka kwa Sultani." Wakampeleka. Sultani akamwuliza, "Kwa nini ulikuwa mkaidi na sasa umekwiba maji." Sungura akasema, "Nifunge na ntakufa." Sultani akasema, "Na afungwe." Sungura akasema, "Usinifunge kwa kamba ya mnazi, nifunge kwa mgomba na nitakufa marra moja ukinitupa juani." Wakamfu-

MASOMO YA PILI

nga wakamtupa juani. Akalala hatta **saa sita**, wakasikia mgomba ukikatika, wakamwambia Sultani, "Sungura atakata mgomba." Sungura akasema, "Niache nitakufa." Saa saba akajikakamua sana, mgomba ukakatika, akakimbia sana, wasiweze kumkamata tena.

kudhuru	kuongeza	kulekule
assubuhi	mpumbavu	kisima
kuonekana	mgomba	kujikakamua
kukatika		

KADHI NA MTOTO.

PALIKUWA mtu mmoja na babae, akazaa mtoto mmoja. Bassi babae akafa. Bassi akamwambia mtoto, "Nadhiri yako, walakini uchimbe shimo uingie mwenyewe." Akafa babae. Hatta siku moja akatokea kadhi, na kadhi yule ataka kubwa kwao. Bassi kadhi akatumwa na Sultani kufanya suluhu mji mgine, kadhi akamwona mtoto huyu njiani akichimba shimo. Kadhi akamwambia mtoto, "Kwani unachimba shimo?" Mtoto akanena, "Nachimba shimo kuingia mwenyewe." Bassi mtoto akafukia shimo wakaenda zao mjini. Yule kadhi aka-

mwambia mzee wa mji, "Nipe mtoto nimchukue kwangu." Mzee akamwambia, "Mchukue yatima." Akamchukua hatta kwao, wakakaa kitako nyumbani. Hatta siku moja Kadhi akaitwa na Sultani, Sultani akamwambia Kadhi, "Nataka kubwa, hukumu kama Mungu, kana hukuhukumu 'takuua." Kadhi akapotea akili, akamwambia mtoto, "Nitauawa." "Kwa nini?" mtoto akauliza. Akamwambia, "Nimeambiwa mambo mazito." Mtoto akanena "Takwenda mimi nikahukumu kama Mungu." Wakaenda zao hatta kwa Sultani. Bassi walipofika kwa Sultani, Akamwambia asikari, "Mfungeni," wakamfunga. Akanena, "Sasa Sultani mimi." Tena akanena "Mfungueni." Akanena, "Twae Sultani wako." Akanena, "Hivi ndivyo anavyohukumu Mungu." Yule Sultani akampa lakki reale, Sultani akamwambia mtoto, "Ahasanta."

Yule mtoto akachukua lakki reale, akampa Kadhi, Kadhi akala, asimpe mtoto.

Siku ya pili Sultani akamwita Kadhi, akamwambia "Nataka hukumu, ndege wawili wanagombana, kama hukuhukumu ntakuchinja." Kadhi akaenda nyumbani akaogopa. Mtoto yule akamwambia, "Una nini?" Kadhi akamwambia, "Mambo mazito sana. Kama siku hukumu ndege wawili ntachinjwa, na muhulla

siku moja." Mtoto akamwambia, " Ntahukumu mimi." Akaenda mtoto kwa Sultani. Sultani akamwambia mtoto, " Hukumu ndege wawili." Akamwambia, " Nipe bunduki." Akaweletekeza bunduki kwa mbali, ikalia bunduki, wakaruka, mmoja akarudi, mmoja akaenda zake. Sultani akauliza, " Maana yake nini?" Yule Mtoto akanena, " Ndege mmoja aliokwenda zake alikuwa na mkewe, mkewe akafa, na kufa kwake ana shaka, amekufa kwa hamu za ndege mwensiwe aliyerudi, bassi akanena, ' Takwenda mbele ya Sultani, atahukumu kama sheria.' " Sultani akampa mtoto laki reale akamwambia " Ahasantu."

Mtoto akampa Kadhi fedha. Bassi Kadhi yule akasahau fadhili. Mkewe Kadhi akamwambia, " Bwana wangu, mtoto mbaya huyu, asadhalii tumue." Kadhi akanena, " Kwa nini? Akili nyingi mtoto huyu, utamuaje?" Akamwambia, " Yule mtu anaochinja ng'ombe, tumpe fedha ujira wake, atamua." Yule Kadhi akamwambia mchinja ng'ombe, " Twaa reale mia, mue mtoto wangu." Mchinja ng'ombe akamwulia, " Nitamchinjaje?" Akamwambia, " Nitamtuma kukwambia, ' Kazi imekwisha mchinja?'" Yule mchinja ng'ombe akamwambia Kadhi, " Nipe khati ya mkono wako." Kadhi akampa khati. Bassi mchinja ng'ombe

akamwambia, "Mlete mtoto." Hatta assubuhi Kadhi akamtuma mtoto, akampa reale akamwambia, "Kanunue nyama." Mtoto akaenda kununua nyama ; alipofika njiani akakuta watu saba wana ngamia mmoja. Wakamwambia mtoto yule, "Ngamia huyu thamani yake reale nane, bassi sisi tuna saba, twataka moja, tukipata moja tutamchinja." Mtoto akafikiri, akanena moyoni mwake, "Mimi killa siku hununua nyama ya reale, nayo huwa kidogo. Bassi leo nitajitia shirikani hapa, taenda nikapata baraka kwa baba wangu." Bassi wakajiharakisha kuchinja ngamia, ikapata saa tano. Kadhi akamtuma mtoto wake mwingine kumtazama mchinja ng'ombe kama kazi imekwisha. Mchinja ng'ombe akamwambia, "Njoo," akaenda mtoto. Akamchinja akamtia shimonii. Na yule mtoto mwingine akachukua nyama ya ngamia akapeleka nyumbani. Kadhi alipomwona machozi yakamtoka akasikitika. Na mkewe Kadhi analia, na nyumbani kumeingia huzuni na msiba. Yule mtoto akanena moyoni mwake, "Si burre, hapa pana neno bayo, lakini nimeleta nyama nyingi, hakufurahi wala sikupata baraka." Bassi akatokea kijakazi, akamwambia kibwana, "Kuna msiba nyumbani." Yule kijana akasema, "Msiba wa nini?" Akasema, "Nduguyo kachinjwa na mchinja nyama, na

msiba huu walikuwa wako." Mtoto akasema, "Marahaba, ahsanti kijakazi wewe, hukustahili kuwa mtumwa." Bassi mtoto akanenda kwa Sultani, akashtaki, akampa habari yote iliyo-mpata yule mtoto. Mtoto akamwambia Sultani, "Nalipewa wusia na baba wangu, akanambia, nadhiri yako, uchimbe shimo kuingia mwenyewe, bassi leo uhukumu na Kadhi." Sultani aka-mwita Kadhi akamchinja, na mali yake akatwaakampa mtoto pamoja na ukadhi, na kijakazi akawa huru. Hii ndiyo maana ya hadithi ya mchimba shimo kuingia mwenyewe.

nadhiri	kadhi	suluhu
yatima	ahasanta	lakki
kuchinja	muhulla	fadhili
ujira	ng'ombe	khati
kusikitika	ngamia	shirikani
kuharakisha	kijakazi	kushtaki

RICHARD CLAY & SONS, LIMITED,
BREAD STREET HILL, E.C., AND
BUNGAY, SUFFOLK.

This book should be returned
the Library on or before the last date
stamped below.

A fine of five cents a day is incurred
by retaining it beyond the specified
time.

Please return promptly.

FEB 18 65 H

SO 6498

CANCELLED

MAY 27 67 H

S 2700



Digitized by Google